# 03- Aina Za Hajj

Anasema Allaah (سبحانه وتعالى):

﴿ ٱلۡحَجُّ أَشۡهُرٞ مَّعۡلُومَٰتٞۚ فَمَن فَرَضَ فِيهِنَّ ٱلۡحَجَّ فَلَا رَفَثَ وَلَا فُسُوقَ وَلَا جِدَالَ فِي ٱلۡحَجِّۗ وَمَا تَفۡعَلُواْ مِنۡ خَيۡرٖ يَعۡلَمۡهُ ٱللَّهُۗ وَتَزَوَّدُواْ فَإِنَّ خَيۡرَ ٱلزَّادِ ٱلتَّقۡوَىٰۖ وَٱتَّقُونِ يَٰٓأُوْلِي ٱلۡأَلۡبَٰبِ ١٩٧ ﴾

**((Hajj ni miezi maalumu. Na atakayekusudia kuhiji (akahirimia), basi asifanye tendo la ndoa wala ufasiki wala mabishano katika Hajj. Na lolote mlifanyalo katika ya kheri Allaah Analijua. Na chukueni masurufu. Na hakika bora ya masurufu ni taqwa. Na nicheni Mimi enyi wenye akili!))**[1]

Wamekubaliana Wanachuoni kwamba miezi ya Hajj ni Shawwaal, Dhul-Qa'dah na Dhul-Hijjah. Kwa hiyo mtu anaweza kuelekea Makkah katika miezi hiyo.

عَنْ جَابِرٍ (رضي الله عنه) عَنْ النَّبِيّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ قَالَ: ((**لَا يَنْبَغِي لِأَحَدٍ أَنْ يُحْرِم بِالْحَجِّ إِلَّا فِي أَشْهُر الْحَجّ**))

Imepokelewa toka kwa Jaabir (رضي الله عنه) kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) amesema: **((*Haipasi kwa yeyote aingie katika Ihraam isipokuwa katika miezi ya Hajj*))**[2]

Kuna aina tatu za Hajj; *At-Tamattu', Al-Qiraan, Al-Ifraad*. Aina hizo zinategemea hali ya mtu na nchi anayoishi.

## *At-Tamattu'* - التَّمَتُّع

Ni aina ya Hajj kwa niyyah ya kufanya 'Umrah kisha Hajj. Anayetekeleza huitwa *Al-Mutamatti'*.

Haji atavaa Ihraam ya 'Umrah tu wakati wa miezi ya Hajj, (anapokwenda Makkah mapema) ambayo inamaanisha kwamba atakapofika Makkah atafanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* ya 'Umrah. Kisha atanyoa au kukata

[1] Al-Baqarah (2: 197).
[2] Tafsiyr Ibn Kathiyr.

nywele, hapo atakuwa amemaliza 'Umrah, na atavua Ihraam yake na kusubiri siku ya *Tarwiyah* ambayo ni siku ya tarehe 8 Dhul-Hijjah. Siku hiyo Haji atavaa nguo zake za Ihraam kwa ajili ya Hajj tu na atatekeleza yote yanayompasa kufanya.

*Hajj At-Tamattu'* Inatekelezwa kwa mpangilio ufuatao:

Utakapofika *Miyqaat*, utaingia katika Ihraam kwa niyyah ya 'Umrah.

- Utekeleze 'Umrah ndani ya miezi hiyo ya Hajj katika mwaka huo, na lazima umalize kabla ya tarehe 8.
- Ufanye *Twawaaf* ya 'Umrah moja kwa moja, hutakiwi kuanza na *Twawaaful-Quduwm*.
- Ufanye *As-Sa'-y* ambayo ni ya 'Umrah. (*As-Sa'-y* ya Hajj inatekelezwa pamoja na *Twawaaful-Ifaadhwah*).
- Utakata au unyoe nywele (kwa mwanamume), ikiwa una masiku ya kutosha hadi nywele ziote tena kwa ajili ya kunyoa utapomaliza Hajj; na ni vyema kunyoa kuliko kukata, kwani ina thawabu zaidi.
- Baada ya hapo utakuwa umesh'amaliza kutekeleza 'Umrah na umeshatoka katika Ihraam, na hutakuwa na vikwazo vyovyote vya Ihraam.
- Itakapofika tarehe 8 Dhul-Hijjah utaingia katika Ihraam tena kwa niyyah ya Hajj, na kuelekea *Minaa*.
- *Al-Mutamatti'u* lazima achinje. Ikiwa huna uwezo, unatakiwa kufunga siku kumi; tatu unapokuwa Hajj, na saba unaporudi nchini mwako. Hii kwa wanaoishi nchi za nje.

﴿ فَمَن تَمَتَّعَ بِٱلۡعُمۡرَةِ إِلَى ٱلۡحَجِّ فَمَا ٱسۡتَيۡسَرَ مِنَ ٱلۡهَدۡيِۚ فَمَن لَّمۡ يَجِدۡ فَصِيَامُ ثَلَٰثَةِ أَيَّامٖ فِي ٱلۡحَجِّ
وَسَبۡعَةٍ إِذَا رَجَعۡتُمۡۗ تِلۡكَ عَشَرَةٞ كَامِلَةٞۗ ﴾

**((basi mwenye kutekeleza 'Umrah (katika miezi ya Hajj) kisha Hajj, basi achinje mnyama aliye mwepesi. Na asiyepata (mnyama), afunge *Swiyaam* siku tatu katika Hajj na (siku) saba mtakaporejea. Hizo ni (siku) kumi timilifu))**[3]

[3] Al-Baqarah (2:196).

Ama wakaazi wa Makkah hawatakiwi kutekeleza aina hii ya Hajj kwa dalili:

﴿ ذَٰلِكَ لِمَن لَّمْ يَكُنْ أَهْلُهُۥ حَاضِرِى ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ۚ ﴾

**((Hayo ni kwa ajili ya yule ambaye watu wake hawaishi karibu na Al-Masjidil-Haraam))**[4]

[4] Al-Baqarah (2:196).

# Chati Ya Hajj Tamattu’

### *Al-Qiraan* – الْقِران

Ni aina ya Hajj inayochanganywa na ‘Umrah kwa niyyah moja, bila ya kutoka katika Ihraam. Anayetekeleza huitwa *Al-Qaarin*.

Haji atavaa Ihraam kwa niyyah ya 'Umrah na Hajj au anavaa kwanza Ihraam ya 'Umrah, kisha anatia niyyah ya Hajj kabla ya *Twawaaful-Ifaadhwah*. Vitendo vinavyowajibika kwa anayefanya Ifraad ni sawa sawa na anayefanya Qiraan, isipokuwa tu mwenye kufanya Qiraan inampasa achinje na mwenye kufanya Ifraad haimpasi kuchinja.

Inatekelezwa kwa mpangilio ufatao:

- Unapofika *Miyqaat* ingia katika Ihraam kwa niyyah ya ‘Umrah na ya Hajj.
- Lazima uwe na mnyama wa kuchinja kama walivyokubaliana Wanachuoni kuwa ni sharti ya aina hii ya Hajj. Na ikiwa huna basi itabidi ubadilishe niyyah na utekeleze Hajj ya *Tamattu’*. Kwa hiyo aliyekuwa na mnyama hawezi kubadilisha niyyah bali itabidi atekeleze taratibu za aina hii ya Hajj.
- Unaweza kufanya *As-Sa’-y* ya Hajj pamoja na hiyo *Twawaaful-Quduwm* au unaweza kuichelewesha *As-Sa’-y* ukafanya baada ya *Twawaaful-Ifaadhwah*. Lakini kuifanya *As-Sa’-y* pamoja na *Twawaaful-Quduwm* ni bora zaidi.
- Lazima ubakie katika Ihraam siku zote tokea unapofika Makkah mpaka umalize taratibu za Hajj.
- Wakaazi wa Makkah hawatakiwi kutekeleza aina hii ya Hajj.

### *Al-Ifraad* - الإفراد

Ni aina ya Hajj inayotekelezwa bila ya 'Umrah, nayo huwa kwa niyyah moja tu ya Hajj. Anayetekeleza huitwa *Al-Mufrid*.

Haji atavaa Ihraam kwa ajili ya Hajj pekee. Atakapofika Makkah atafanya *Twawaaful-Quduwm* akipenda (kwani ni Sunnah kwake) kisha ataelekea *Minaa*. Hanyoi wala kukata nywele zake kwani hatoki kwenye Ihraam yake, bali atabakia katika Ihraam mpaka 'amalize kurusha vijiwe katika *Jamrah Al-'Aqabah* siku ya 'Iyd. Anaruhusiwa kuchelewesha *As-Sa'-y* yake ya Hajj mpaka 'amalize *Twawaaful-Ifaadhwah*.

Unapofika *Miyqaat* ingia katika Ihraam kwa niyyah moja tu ya Hajj.

- Huhitaji mnyama wa kuchinja.
- Ukifika Makkah, ufanye *Twawaaful-Quduwm* ukipenda kwani unaweza kwenda moja kwa moja kutoka *Miyqaat* kuelekea *Minaa* tarehe 8 Dhul-Hijjah.
- Unaweza kufanya *As-Sa'-y* ya Hajj pamoja na hiyo *Twawaaful-Quduwm*? Hivyo utakuwa sawa na *Al-Qaarin* kuhusu kubadilisha niyyah kufanya ya *At-Tamattu'* isipokuwa wakaazi wa Makkah.
- Lazima ubakie katika Ihraam siku zote, tokea unapofika Makkah mpaka utakapomaliza taratibu za Hajj.
- Aina hii ya Hajj inawapasa watekeleze wakaazi wa Makkah au walio karibu na maeneo ya *Miyqaat*.
- Ikiwa muda upo, *Al-Mufrid* anaweza kubadilisha niyyah kutoka *Al-Ifraad* kufanya ya *Al-Qaarin* au ya *At-Tamattu'*.

Aina ya Hajj iliyo bora kabisa katika hizo ni ya *At-Tamattu'* kwa sababu ya usahali wa kutokubakia katika Ihraam masiku mengi. Pia Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alisisitiza wafuasi wake waitekeleze kama alivyosimulia Abu Sa'iyd (رضي الله عنه):

**"خَرَجْنَا مَعَ رَسُول اللَّه صَلَّى اللَّه عَلَيْهِ وَسَلَّمَ نَصْرُخ بِالْحَجِّ صُرَاخًا فَلَمَّا قَدِمْنَا مَكَّة أَمَرَنَا أَنْ نَجْعَلهَا عُمْرَة إِلَّا مَنْ سَاقَ الْهَدْي، فَلَمَّا كَانَ يَوْم التَّرْوِيَة وَرُحْنَا إِلَى مِنى أَهْلَلْنَا بِالْحَجِّ"**

**"**Tulitoka pamoja na Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) wakinyanyua sauti zao (kwa *Talbiyah*) kwa ajili ya Hajj. Tulipofika Makkah alituamrisha tufanye

'Umrah isipokuwa ambaye amechukua *Hadyi* (mnyama wa kuchinja). Ilipofika siku ya *Tarwiyah* tukaenda *Minaa* tukatia niyya ya Hajj.[5]

Hata kama Mahujaji akitia niyyah ya kufanya Qiraan au Ifraad, anaruhusiwa kubadilisha niyyah yake kuingia katika Hajj ya *Tamattu'*. Na anaweza kufanya hivi hata kama baada ya kufanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alipofanya *Twawaaf* na *As-Sa'-y* mwaka wa *Hajjatul-Wadaa'i* (Hajj ya kuaga) pamoja na Maswahaba zake, aliamrisha wote ambao hawakuleta mnyama kwa ajili ya kuchinja, wabadilishe niyyah zao za Hajj na kutia niyyah ya 'Umrah, wakate nywele zao, na wavue Ihraam mpaka Hajj. Akasema:

((**فَلَوْلاَ أَنِّيسُقْتُ الْهَدْيَ لَفَعَلْتُ مِثْلَ الَّذِيأَمَرْتُكُمْ بِهِ**)) البخاري

***((Ingelikuwa sikuleta mnyama ningelifanya hivyo nilivyokuamrisheni mfanye***))[6]

**Yanayofahamika Sivyo Na Yanayotendeka Kimakosa**

- Kwamba mwezi wa Hajj pekee ndio zinaanza *Manaasik* za Hajj na hali miezi ya Hajj inaanzia Shawwaal mpaka siku za Hajj zenyewe.

- Kudhania kwamba Hajj ya *Al-Qiraan* ni bora kuliko ya *At-Tamattu'* kwa sababu Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) alitekeleza ya *Al-Qiraan*. Rasuli (صلى الله عليه وآله وسلم) aliamrisha na kupendekeza Hajj ya *At-Tamattu'*:

  عن جابر بن عبد الله (رضي الله عنه) أنه حجَّ مع النبي صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يوم ساق البُدن معه، وقد أهلُّوا بالحجِّ مفرداً، فقال لهم: ((**أَحِلُّوا مِنْ إحْرامِكُم بِطَوَافٍ بالبَيْتِ، وبَيْنَ الصَّفَا والْمروَة، وقَصِّرُوا، ثُمَّ أقِيمُوا حَلالاً، حَتَّى إذَا كَانَ يَومُ التَّرْوِيَةِ، فأهِلُّوا بالحَجِّ واجْعَلُوا التي قَدِمْتُم بها مُتْعَةٌ**)) فقالُوا: كَيْفَ نَجْعَلُها مُتْعَةً وَقَدْ سَمَّيْنَا الحَجَّ؟ فقال: ((**افْعَلُوا مَا آمُرُكُم به، فَلَوْلا أنى سُقْتُ الهَدْى، لَفَعَلْتُ مِثْلَ الَّذي أَمَرْتُكُم بِهِ**))

---

[5] Muslim.
[6] Al-Bukhaariy.

Imepokelewa toka kwa Jaabir bin 'Abdillaah (رضي الله عنه) kwamba alihiji pamoja na Nabiy (صلى الله عليه وآله وسلم) ambaye alichukua *Al-Hadyi* (mnyama wa kuchinja) na kwamba walitia niyyah ya kufanya Hajj ya *Ifraad*. Akawaambia: ***((Jitoeni Ihraam baada ya kufanya Twawaaf na baada ya As-Sa'-y baina Asw-Swafaa na Al-Mar-wah, kisha mkate nywele zenu. Kisha mbakie Makkah mkiwa mmeshajivua katika Ihraam mpaka siku ya Tarwiyah (8 Dhul-Hijjah) mtatia*** **niyyah** ***ya Hajj kisha mtafanya 'ibaadah zenu kuwa ni Tamattu')*** ) Wakauliza: "Vipi tufanye *Tamattu'* na hali tumeshaitilia niyyah ya Hajj (*Al-Ifraad*)"? Akasema: ***((Fanyeni nilivyokuamrisheni, kwani ingelikuwa sikuleta Al-Hady, ningelifanya kama nilivyokuamrisheni))***[7]

---

[7] Al-Bukhaariy.